JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

*Unapojibu tafadhali taja;-*
**Kumb. Na. TDC.L.40/31/61**

**Tarehe 03/06/2026**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi za Mkataba; Daktari II Nafasi 10, Mtaalamu wa Usingizi Nafasi 01,Afisa Muuguzi Msaidizi II nafasi 30,Tabibu II Nafasi 09,Mteknolojia Dawa II Nafasi 02,Mwalimu III C Historia 05,Mwalimu III C Kingereza O7,Mwalimu III C Jiografia 02 na Mwalimu III C Biashara 02.

### 1.0 DAKTARI II (NAFASI 10)

**a) SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa mwenye shahada ya Udaktari/Daktari wa meno toka vyuo vikuu vinavyo tambuliwa na serikali.

**b) Kazi na majukumu:**

(i) Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali katika fani husika.
(ii) Kupanga, kusimamia na kutathimini huduma katika wilaya au mikoa
(iii) Kufundisha wanafunzi katika vyuo vya afya vilivyo eneo lake la kazi
(iv) Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa
(v) Kutayarisha elimu ya kujiendeleza ya watumishi wa afya.
(vi) Kufundisha na kuelekeza watumishi walio chini yake
(vii) Kusimamia wafanyakazi walio chini yake.
(viii) Kubuni, kuendesha na kutathimini utafiti na kusambaza matokeo
(ix) Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake

(x) Kutoa huduma za outreach katika kanda

(xi) Kutoa huduma za medical legal

(xii) Kushiriki katika kutengeneza na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali juu ya afya

(xiii) Kushauri wizara kuhusu uendeshaji wa shughuli za afya nchini.

(xiv) Kushiriki katika kamati ya jopo la madaktari (medical board) kwa ajili ya kustaafisha wafanyakazi kwa matatizo ya kiafya.

(xv) Kutayarisha mitaala ya elimu ya kujiendeleza ya watumishi wa afya.

(xvi) Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya

(xvii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**MSHAHARA**

Daktari wa Mkataba atalipwa posho ya Tsh.900,000/= kwa mwezi.

## 2.0 MTAALAMU WA USINGIZI -(NAFASI 01)

***a)* Sifa za kuajiriwa moja kwa moja**

Kuajiriwa wenye Utaalamu wa ganzi na Dawa za Usingizi mwenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi/Tabibu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

***b)*Kazi na Majukumu:**

I. Kumchunguza mgonjwa kabla ya upasuaji
II. Kutoa dawa za usingizi
III. Kufuatilia Mgonjwa wakati wa upasuaji
IV. Kutdhibiti maumivu
V. Kumhudumia Mgonjwa baada ya upasuaji
VI. Kushiriki katika huduma za dharura
VII. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi

**MSHAHARA**

Mtaalamu wa Usingizi wa Mkataba atalipwa posho ya Tsh. 600,000/= kwa mwezi.

## 3.0 AFISA MUUGUZI MSAIDIZI II-(NAFASI 30)

***a)* Sifa za kuajiriwa moja kwa moja**

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

**b) Kazi na Majukumu:**

(i) Kutoa huduma za uuguzi
(ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya.
(iii) uwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake
(iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
(v) Kutoa huduma za kinga na uzazi
(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**MSHAHARA**

Afisa Muuguzi Msaidizi II wa Mkataba atalipwa posho ya Tsh.250,000/= kwa mwezi.

**4.0 TABIBU II-(NAFASI 09)**

***a) Sifa za kuingilia moja kwa moja:***
Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya Tabibu/Tabibu Meno kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

***b) Kazi na majukumu:***

(i) Kazi zote zinazofanywa na Tabibu Msaidizi
(ii) Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
(iii) Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo
(iv) Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi
(v) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya za Mfuko wa Afya ya Jamii
(vi) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
(vii) Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji
(viii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

**MSHAHARA**

Afisa Tabibu II wa Mkataba Atalipwa posho ya Tsh.250,000/= kwa mwezi.

**3.2 MTEKNOLOJIA DAWA II (NAFASI 02)**

**(a) Sifa za kuingilia moja kwa moja:**
Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika fani Dawa kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

***b)Kazi na majukumu:***

(i) Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
(ii) Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi
(iii) Kuchanganya dawa
(iv) Kuhifadhi dawa na vifaa tiba
(v) Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa
(vi) Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi
(vii) Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.
(viii) Kuratibu kazi za kamati ya dawa ya hospitali
(ix) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
(x) Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi
(xi) Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.
(xii) Kusimamia utendaji wa kazi watumishi walio chnini yake
(xiii) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
(xiv) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake,

**MSHAHARA**

Mteknolojia Dawa II wa Mkataba atalipwa posho ya Tsh.250,000/= kwa mwezi.

**3.0 MWALIMU III B NA III C (NAFASI 16)**

Kwa masomo ya Historia,Kingereza,Jiografia na Biashara.

**3.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa mwenye Shahada ya Ualimu katika masomo ya Sanaa na Biashara.

**4.2 MAJUKUMU YA KAZI**

i. Kuandaa azimio la kazi,maandalio ya masomo,nukuu za masomo na Mpango kazi wa majukumu mengine aliyokabiziwa;
ii. Kutengeneza na kufaraghua zana za kufundishia na kujifunzia;
iii. Kufundisha,kufanya tathmini na kutunza kumbukumbu za maendeleo ya Wanafuzi
iv. Kusimamia na kufuatilia mahudhurio ya Wanafunzi Shuleni na darasani;
v. Kusimamia malezi ya Wanafunzi kiakili,kimwili,kiroho na kutoa ushauri nasaha na unasihi;
vi. Kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kuhusu maendeleo ya Elimu;

vii. Kusimamia na utunzaji wa vifaa na mali za Shule

viii. Kazi nyingine atakazopangiwa na Mwalimu Mkuu kulingana na majukumu ya Shule.

## MSHAHARA

Mwalimu wa Mkataba atalipwa posho ya Tsh.300,000/= kwa mwezi.

## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 na usiozidi miaka 45

ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha ulemavu walionao.

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani inayotumika,namba za simu zinazopatikana na anuani ya barua pepe(E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho cha elimu na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma / Certificate- Cheti cha Mtihani wa kidato cha nne na cha Sita, Computer Certificate- Vyeti vya kitaaluma (Proffessional Certificate from Respective Boards).

v. Wasailiwa watakaowasilisha Testimonials, Provisional Results,Statement of results, hati za matokeo za kidato cha IV na VI ( form V and VI results slips) **HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI.**

vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika ( TCU,NECTA na NACTVET).

vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokua kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

viii. Waombaji wa kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na.CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.

ix. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.

x. Wasailiwa ambao majina yao yanatofautiana katika nyaraka zao wanapaswa kuwasilisha Hati ya Kiapo cha Kubadili Jina (Deed Poll)iliyosajiliwa na Wizara ya Ardhi.

xi. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 17 Juni, 2026.

**Barua zote zitumwe kwa njia ya posta kwa**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru**
**48 Barabara ya Nalasi ,S.L.P 275,57682**
**Tunduru.**

Tangazo hili limetolewa na,

Chiza C. Marando
**MKURUGENZI MTENDAJI(W)**
**TUNDURU**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
TUNDURU